

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**



**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU VYOMBO VYA HABARI
VINAVYOTANGAZA MATOKEO YA UTEUZI WA WAGOMBEA WA
UBUNGE NA UDIWANI**

Dodoma, Jumatano 26 Agosti, 2020

Jana Agosti 25, 2020, Tume ya Taifa ya Uchaguzi imekamilisha zoezi la uteuzi wa wagombea wa Kiti cha Rais na Makamu wa Rais, Ubunge na Udiwani nchi nzima. Wakati Tume ikiwa haijatao taarifa yoyote juu ya zoezi hili muhimu, tayari vyombo vya habari kadhaa vimeanza kutangaza matokeo ya uteuzi huo. Mathalan, Televisheni ya Clouds asubuhi hii imetoa matangazo ya wabunge inaodai kuwa wameshinda kwa kuwa wamepita bila kupingwa majimboni mwao. Kitendo hiki ni kinyume cha sheria za Uchaguzi na kina maana ya kupoka uhuru na majukumu ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 40 (2) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, pingamizi linaweza kuwekwa kwa mgombea wa ubunge kama zuiio kwa mgombea aliyeteuliwa kuanzia saa kumi kamili (10:00) jioni siku ya uteuzi hadi saa kumi kamili (10:00) jioni siku inayofuatia baada ya siku ya uteuzi. Kabla muda huo wa kuweka pingamizi haujaisha, tayari vyombo vya habari vimeanza kutangaza matokeo hayo kinyume cha sheria. Kitendo hiki kinaweza kuchochea vurugu na uhasama miongoni mwa wananchi.

Tume inaviasa vyombo vya habari kuzingatia sheria na maadili ya kazi zao. Tume itachukua hatua kali za kisheria kwa chombo chochote kitakachoonekana kwenda kinyume na sheria, kanuni na taratibu za Uchaguzi.


Imetolewa na:

Mkurugenzi wa Uchaguzi

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI